Mzao Teule

(A Chosen Generation)

Na

J. D Logan

Mzao Teule

(A Chosen Generation)

Na

J. D Logan

Novemba 5, 2011

Mzao Teule

Kifungu: 1 Petro 2:9-12

"…ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu; ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepate rehema. Wapenzi nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tama za mwili zipinganazo na roho. Mwe na mwenendo mzuri kati ya mataifa, ili iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamampo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa."

Uaminifu na Uhusiano

Kifungu chetu kinaongelea nafasi ya Mkristo katika maisha yake ya kidunia, pamoja na uhusiano wake na Mungu, na dunia. Inatufundisha kuhusiana na nafasi yetu mbinguni, serikali iliyoteuliwa, ambaye mkuu wake ni Mungu, ambaye anatudai uaminifu wetu wote, na heshima ambayo tunatakiwa kutoa kwa serikali ya dunia, ambayo inatii ile ya Mungu.

Ukikumbuka kwamba maneno yanatakiwa kutafsiriwa, itakuwa vyema kupitia tariri hii kutafsiri maana ya maneno tofauti tofauti ya kifungu chetu. Nimetumia vitabu vifuatavyo vya wasomi: Kitabu cha Thayer Kiyunani – Kiingereza, Fafanuzi ya Vine ya maneno ya Biblia, na msisimko wa Strong's Konkodensi ya Biblia. Hakuwezi kukawa na uanafunzi bora kuliko haya.

Mzao Mteule

Mzao unatafsiriwa kama "genos, kuzaliwa, nchi (-mmwanamume), tofauti, mzao, vitukuu, taifa, malimbuko, akiba."

"Kwa sababu hiyo nawaambia Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu nao watapewa taifa linguine lenye kuzaa matunda yake." (Mat. 21:43)

Kabla ya Kristo kuja, ufalme wa Mungu ulikuwa unamilikiwa na Wayahudi, lakini ilitolewa kwao wakapewa "mafia" tofauti. Taifa hili linaelezwa kwamba ni *teule* (*eklektos*) ambayo hutafsiriwa kama "chaguliwa", "pendelewa".

Kuwa taifa, kunatakiwa kuwe na serikali ili kuweza kuweka madaraka miongoni wa wananchi, la sivyo vurugu zitatawala juu ya serikali. Ni mapenzi ya Mungu kwamba kusiwe na vurugu katika taifa, bali afadhali amani. "*Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali*

wa amani; vile vile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu." (1 Kor. 14:33)

Mungu, Mfalme

Paulo anaeleza uasili wa ufalme huu na ukuu wake. "*Mungu mmoja naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.*" (Efe. 4:6)

Mungu kama ilivyo wajibu wake, amemchagua Mwanaye, Yesu Kristo kuwa kichwa cha ufalme wake hadi wakati wa kuisha kwa kila kitu. "*Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa.*" (Efe. 1:22)

Sisi ni "*ukuhani mkuu*" kupitia uhusiano wetu na Mungu, Mfalme wetu.

Taifa Juu Ya Mabega Yake

Isaya alitabiri kuhusu taifa lake jipya na serikali yake. "*Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake, naye ataitwa jina lake mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu Baba wa milele, mfalme wa amani.*" (Isa. 9:6) "*Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki tangu sasa na hata milele. Wivu wa BWANA wa majeshi ndio utakaotenda hayo.*" (Isa. 9:7)

Watendaji

Kuangalia taifa la Mungu, Yesu alitengeneza nafasi ambazo zinajazwa na watu wenye sifa ambao wangechukua madaraka yao kwake. "*Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe.*" (Efe. 4:11-12).

Huu Ndiyo Mpangilio Mfupi Wa Serikali Ya Kristo, Mkuu Aliyechaguliwa Katika Ufalme wa Mungu

Utaifa

Wakristo, kama watu wa Mungu, ni wahitimu "raia" wa taifa. "*Kwa maana sisi wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo.*" (Fil. 3:20)

Neno *wenyeji* katika kifungu hiki inatoka katika "*politeuma*" ikimaanisha "jamii, ie raia" Paulo anatuambia kwamba <u>uraia</u> wetu uko mbinguni (ambako mkuu wetu wa serikali alipo).

Zaidi sana, anatuambia, "*Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo, ili nikija na kuwaonya ninyi, au nisipokuwapo niyasikie mambo yenu kama mnasimama imara katika Roho moja, kwa moyo mmoja mkiishindania imani ya Injili.*" (Fil. 1:27)

Katika kifungu hiki neno ni "*politeuomai*" ikimaanisha "kuwa kama raia". Tabia zetu katika dunia hii zinapaswa kuwa bora kama raia "mzao mteule (taifa)".

Hapa, Hakuna "Mji unaoendelea"

Sisi ni raia wa taifa la mbinguni pamoja na uraia wetu mbinguni, kwa sababu hapa hatuna makao ya milele. "*Wapenzi nawasii kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tama za mwili zipinganazo na roho…*" (1 Pet. 2:11). "*Hawa wote wakafa katika imani wasijazipokea zile ahadi bali wakaziona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kwamba walikuwa wageni na wasafiri juu ya nchi.*" (Ebr. 11:13)

Kama sisi ni wapitaji na wageni katika maisha yetu ya sasa, inafuata kwamba uraia wetu hauko hapa miongoni mwa serikali na taifa la wanadamu. "*Maana hapa hatuna <u>mji udumuo</u>, bali twautafuta ule ujao.*" (Ebr. 13:14)

"*Udumuo*" (*meno*) inatolewa "…sehemu iliyotolewa, serikali, uhusiano: kaa, ishi. Hivyo, sisi ni raia ambao sehemu yetu ya makazi siyo hapa katika ulimwengu huu, bali mbinguni pamoja na mfalme wetu.

Watu wa Milki

Katika kifungu chetu, Wakristo wanaelezwa kama watu wa "*milki*". Hatuongelei kama "*watu*" (kwa ujumla) bali kama "*milki*" (kama watu wa Irish). Ana maanisha nini juu ya hili? Neno "*milki*" inatafsiriwa kama "kununua"

"*…Mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu mliyepewa na Mungu?* ***Wala ninyi si mali yenu wenyewe;"*** (1 Kor. 6:19). "*maana* ***mlinunuliwa kwa thamani****." (1 Kor. 6:20) "m*pate kulilisha kanisa lake Mungu, **alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.**" (Mdo. 20:28).

Tulinunuliwa kwa thamani sana, damu ya Kristo. Tunapaswa kuweka akilini maneno ya Petro. "*Basi kwa kuwa vitu hivi vyote vitafunuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa.*" (2 Pet. 3:11)

Mtumishi mwenzenu katika Kristo,
J D Logan